TAASISI YA UTAFITI WA AFYA ZANZIBAR

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI.

Taasisi ya Utafiti wa Afya Zanzibar (ZAHRI) imeanzishwa kwa Sheria Nambari 5 ya Mwaka 2020 kwa lengo la kuiwezesha na kuongeza nguvu utekelezaji wa majukumu ya Taasisi.

Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Utafiti wa Afya Zanzibar (ZAHRI) kwa niaba ya Bodi ya Wakurugenzi ya Taasisi ya Utafiti wa Afya Zanzibar (ZAHRI), anatangaza nafasi za kazi kwa kada mbali mbali kwa wazanzibari wote wenye sifa na uwezo wa kujaza nafasi hizo kama zilivyoainishwa katika tangazo hili. Nafasi zinazotangaziwa zitakuwa ni kwa kada zifuatazo:-

KADA YA MAAFISA UTAFITI WA AFYA YA BINAADAMU

1. Epidemiolojia Daraja la II (Epidemologist) Nafasi 1

Sifa za Mwombaji

Mwombaji awe na elimu ya Shahada ya uzamili katika fani ya Sayansi ya Epidemioloji katika Chuo kinachotambuliwa na Serikali.

Majukumu

- Kufanya utafiti unaohusu Afya ya binaadamu kwa mujibu wa fani ya mtumishi
- Kuandaa mapendekezo ya Tafiti za Maradhi kwa ajili kupatiwa fedha.
- Kuwasimamia watafiti wasaidizi katika kuandaa kuendeleza mapendekezo ya Utafiti.
- Kushirikiana na watafiti waandamizi katika kutekeleza tafiti zilizopitishwa na kusambaza matokeo yake
- Kuandaa ripoti za utekelezaji wa kazi ikiwemo ripoti ya robo, nusu na ya mwaka;
- Kupanga, kutekeleza na kuendeleza kazi za Utafiti kwa mujibu wa miongozo ya Taasisi;
- Kufanya kazi nyengine zinazolingana na majukumu yake kama atakavyopangiwa na Mkuu wake.

NGAZI YA MSHAHARA -ZPSI – 02

2. Bayoteknolojia Daraja la II (Biotechnologist) Nafasi 1

Sifa za Mwombaji

Mwombaji awe na elimu ya Shahada ya Uzamili ya Biotechnology katika Chuo kinachotambuliwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Majukumu

- Kutunza vifaa na vitendea kazi vya maabara.
- Kusaidia uandaaji waripoti za utekelezaji wa kazi ikiwemo ripoti ya robo, nusu na mwaka.
- Kufanya majaribio ya utafiti na vipimo vya kimaabara
- Kufanya uchunguzi na kusafirisha vinasaba kwa ajili ya uchunguzi zaidi;
- Kuweka na kuhifadhi kumbukumbu za vipimo vilivyofanyika maabara
- Kutoa ushauri katika kuendeleza Utafiti.
- Kushauri wa kitaalamu katika maeneo ya utafiti yenye kuhitaji utaalamu wa vipimo.
- Kufanya kazi nyengine zinazolingana na majukumu yake kama atakavyopangiwa na Mkuu wake.

NGAZI YA MSHAHARA -ZPSI – 02

3. Mwanasosholojia Daraja la II (Sociologist) Nafasi 1

Sifa za Mwombaji

Mwombaji awe na Shahada ya Uzamili ya Sociology kutoka katika Chuo kinachotambuliwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Majukumu.

- Kufanya utafiti unaohusu Afya ya binaadamu kwa mujibu wa fani ya mtumishi
- Kuandaa mapendekezo ya Tafiti za afya ya Jamii kwa ajili ya kupatiwa fedha.
- Kuwasimamia watafiti wasaidizi katika kuandaa kuendeleza mapendekezo ya Utafiti.
- Kushirikiana na watafiti waandamizi katika kutekeleza tafiti zilizo pitishwa na kusambaza matokeo yake
- Kuandaa ripoti za utekelezaji wa kazi ikiwemo ripoti ya robo, nusu na ya mwaka;
- Kupanga, kutekeleza na kuendeleza kazi za Utafiti kwa mujibu wa miongozo ya Taasisi;

- Kufanya kazi nyengine zinazolingana na majukumu yake kama atakavyopangiwa na Mkuu wake.

4 Muuguzi Daraja la II (Clinical Nurse) Nafasi 1

Sifa za Mwombaji

Mwombaji awe na elimu ya Shahada ya Uzamili ya Uuguzi (Clinical Nurse) katika Chuo kinachotambuliwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Majukumu

- Kufanya utafiti unaohusu Afya ya binaadamu kwa mujibu wa fani ya mtumishi
- Kuandaa mapendekezo ya Utafiti wa afya kwa ajili kupatiwa fedha.
- Kuwasimamia watafiti wasaidizi katika kuandaa kuendeleza mapendekezo ya Utafiti.
- Kushirikiana na watafiti waandamizi katika kutekeleza tafiti zilizo pitishwa na kusambaza matokeo yake
- Kuandaa ripoti za utekelezaji wa kazi ikiwemo ripoti ya robo, nusu na ya mwaka;
- Kupanga, kutekeleza na kuendeleza kazi za Utafiti kwa mujibu wa miongozo ya Taasisi;
- Kufanya kazi nyengine zinazolingana na majukumu yake kama atakavyopangiwa na Mkuu wake.

NGAZI YA MSHAHARA -ZPSI – 02

5. Afisa Mazingira Daraja la II (Environmental Science) Nafasi 1

Sifa za Mwombaji

Mwombaji awe na elimu ya Shahada ya Uzamili ya Sayansi ya Afya ya Mazingira ‘Environmental Health Science’ kutoka katika Chuo kinachotambuliwa na Serikali.

Majukumu

- Kufanya utafiti unaohusu Afya ya binaadamu kwa mujibu wa fani ya mtumishi
- Kuandaa mapendekezo ya Tafiti za Afya ya Mazingira kwa ajili ya kupatiwa fedha.
- Kuwasimamia watafiti wasaidizi katika kuandaa kuendeleza mapendekezo ya Utafiti.
- Kushirikiana na watafiti waandamizi katika kutekeleza tafiti zilizo pitishwa na kusambaza matokeo yake

- Kuandaa ripoti za utekelezaji wa kazi ikiwemo ripoti ya robo, nusu na ya mwaka;
- Kupanga, kutekeleza na kuendeleza kazi za Utafiti kwa mujibu wa miongozo ya Taasisi;
- Kufanya kazi nyengine zinazolingana na majukumu yake kama atakavyopangiwa na Mkuu wake.

NGAZI YA MSHAHARA -ZPSI – 02

KADA YA MAAFISA UKUTUBI NA USIMAMIZI WA MACHAPISHO YA UTAFITI

1 Afisa Ukutubi Daraja la II (Documentation Officer) Nafasi 1

Sifa za Mwombaji

Mwombaji awe na elimu ya shahada ya kwanza ya “Library Information Science”/ “Science in Library and Information Management” kutoka katika Chuo kinachotambuliwa na Serikaliya Mapinduzi ya Zanzibar.

Majukumu

- Kutunza vitabu, makabrasha, taarifa za kisayansi na taarifa rejea (reference materials)
- Kuhakikisha kuwa Maktaba ni safi.
- Kushughulikia mifumo ya Library inayohusiana na mifumo ya kieloktroniki.
- Kuhakikisha kuwa Vitabu na Majarida yanawekwa katika mfumo unaohitajika.
- Kuhifadhi machapisho ya Tafiti yanayowasilishwa.
- Kuwasaidia watafiti kupata vitabu, majarida, taarifa na machapisho mengine yatakayowasaidia katika kufanya tafiti zao.
- Kutoa mafunzo na kuwaelekeza wasomaji namna ya kupata taarifa mbalimbali;
- Kuandaa ripoti za utekelezaji wa majukumu ya kazi yake ikiwemo ripoti ya robo, nusu na mwaka.
- Kufanya kazi nyengine zinazolingana na majukumu yake kama atakavyopangiwa na Mkuu wake.

NGAZI YA MSHAHARA -ZPSH – 10

KADA YA MAAFISA MIPANGO NA TAKWIMU

1. Afisa Mipango Daraja la II-Nafasi 2

Sifa za Mwombaji

Mwombaji awe na elimu ya Shahada ya Kwanza katika Fani ya Uchumi (Economics) / Mipango (Planning) / Ufatiliaji naTathmini (M&E) kutoka katika Chuo kinachotambuliwa

na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Majukumu

- Kufanya uchambuzi wa hali halisi ya jambo/eneo husika (Comprehensive situation analysis).
- Kupanga Mipango pamoja na bajeti ya Taasisi.
- Kutayarisha mapendekezo ya Sera na Miradi ya Utafiti katika Taasisi
- Kuchambua na kufanya majumuisho ya Miradi ya Taasisi.
- Kukusanya taarifa na Takwimu zinazohitajika katika kutayarisha Miradi ya Taasisi.
- Kuandaa ripoti za utekelezaji wa majukumu ya kazi yake ikiwemo ripoti ya robo, nusu na mwaka na kuziwasilisha kwa Uongozi wa Taasisi.
- Kufanya kazi nyengine zinazolingana na majukumu yake kama atakavyopangiwa na Mkuu wake.

NGAZI YA MSHAHARA -ZPSH – 10

2. Afisa Takwimu Daraja la II-Nafasi 1

Sifa za Mwombaji

Mwombaji awe na elimu ya Shahada ya Kwanza katika Fani ya Takwimu (Statistics) / Sayansi ya Hesabati na Takwimu / Uchumi na Takwimu kutoka katika Chuo kinachotambuliwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Majukumu

- Kuendeleza mfumo wa kitaifa wa kukusanya na kuratibu Takwimu.
- Kukusanya Takwimu pamoja na kuchukua Takwimu za mifano/vielelezo “sampling”.
- Kukusanya, kusaidia kuchambua na kuwasilisha Takwimu kwa wakuu wake.
- Kusaidia kutengeneza muundo (program) ya kuingiza taarifa za Takwimu katika kompyuta.
- Kuandaa taarifa za utekelezaji wa kazi ikiwemo ripoti ya robo, nusu na mwaka.
- Kufanya kazi nyengine zinazolingana na majukumu yake kama atakavyopangiwa na Mkuu wake.

NGAZI YA MSHAHARA -ZPSH – 10

KADA YA MAAFISA TEKNOLOJIA, HABARI NA MAWASILIANO

1. Afisa Tehama Daraja la II- Nafasi 1

Sifa za Mwombaji

Mwombaji awe na elimu ya Shahada ya kwanza katika Fani ya Computer Science /Computer Engineering/ Networking Engineering/ Information Technology Application and Management kutoka katika Chuo kinachotambuliwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Majukumu.

- Kuandaa na kusimamia Mifumo ya Kielectroniki ya Taasisi
- Kufanya majaribio ya sehemu timilifu za program za Kompyuta (Perform Unit Systems (Module Testing),
- Kufanya majaribio ya mifumo ya TEHAMA (Perform Estaing of System Configurations),
- Kufanya majaribio ya program za Kompyuta kulingana na mahitaji ya watumiaji (Conducting User Acceptance Test),
- Kuweka usalama wa Vifaa vya TEHAMA ndani ya Taasisi.
- Kuzitunza na kuzihakiki taarifa za Taasisi kwa Matumizi ya Serikali.
- Kuweka kumbukumbu za miundombinu ya TEHAMA.
- Kuandaa ripoti za utekelezaji wa kazi ikiwemo ripoti ya robo, nusu na mwaka.
- Kufanya kazi nyengine zinazolingana na majukumu yake kama atakavyopangiwa na Mkuu wake

NGAZI YA MSHAHARA -ZPSH – 10

KADA YA MAAFISA UHUSIANO

1. Afisa Uhusiano Daraja la II-Nafasi 1

Sifa za Mwombaji

Mwombaji awe na elimu ya Shahada ya Kwanza katika Fani ya Uhusiano wa umma (Public Relation)/ Uhusiano wa Kimataifa (International Relation)/Uandishi wa Habari (Journalism), Usimamizi wa Biashara katika masoko (Bussiness Administration in Marketing)/ Mawasiliano ya Umma (Mass Communication) kutoka katika Chuo kinachotambuliwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Majukumu

- Kuitangaza Taasisi kupitia Vyombo vya habari, vipeperushi, redio, magazetiMakala na vyombo vyengine vitakavyoamuliwa na Uongozi wa Taasisi.

- Kupokea malalamiko kwa wadau na wananchi kwa ujumla juu ya utendaji wa Taasisi.
- Kufanya uchunguzi wa malalamiko yaliyowasilishwa kwa Taasisi na kutoa ripoti kamili.
- Kupokea wageni wa Ofisi.
- Kuwasilisha malalamiko sehemu husika.
- Kuandika ripoti za utekelezaji wa kazi ikiwemo ripoti ya robo, nusu na mwaka. na
- Kufanya kazi nyengine zinazolingana na majukumu yake kama atakavyopangiwa na Mkuu wake.

NGAZI YA MSHAHARA -ZPSH – 10

MASHARTI YA JUMLA KWA NAFASI ZOTE

1) Muombaji awe mzanzibari mwenye umri kuanzia miaka 18 na asiyezidi miaka 45

2) Muombaji ambatanishe vivuli vya vyeti vya kumalizia masomo, cheti cha kuzaliwa na kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi (Zan ID)

3) Muombaji wenye vyeti vya vyuo vya nje ya nchi lazima viwe vimebithibitishwa na Kamisheni ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU)

4) Atakaewasilisha Statement of Result au Progressive Report maombi yake hayatazingatiwa

5) Muombaji aambatanishe barua ya maombi ya kazi yenye anuwani ya anaepelekewa (Mkurugenzi Mkuu, Taasisi ya Utafiti wa Afya, Binguni Zanzibar) pamoja na maaelezo binafsi yanayojitosheleza (Detail C.V) yenye anuani na namba ya simu zinazopatikana pamoja na majina ya wadhamini watatu.

6) Muombaji asiombe zaidi ya nafasi moja

7) Maombi yote yatumwe kwenye mfumo wa kielektroniki wa Ajira (Zan Ajira) kupitia anuani https://portal.zanajira.go.tz

8) Muda wa mwisho wa kutuma maombi haya ni tarehe **29/12/2023** ndani ya muda wa kazi.

9) Taarifa zaidi zinapatika katika portal ya Zan Ajira pamoja na Website ya Taasisi

MSISITIZO

Waombaji wote mnasisitizwa kuwa makini mnapowasilisha maombi yenu kwa kuhakikisha masharti na vigezo yanazingatiwa ikiwa ni pamoja na kuambatanishwa nyaraka zote zinazohitajika.